# FURAHIA UDUGU

## KONGAMANO LA TATU LA KIMATAIFA LA UDUGU LA CHAMA CHA MISIONI (UEM)

WUPPERTAL, TAREHE 2-8, JULAI, 2017



# YALIYOMO

Utangulizi ............................ 3

1. Udugu wenye Furaha, Ubunifu, na Ulio Hai ............ 4
2. Upendo kwa Njia ya Matendo... 5
3. Umiliki wa Pamoja .............. 6
4. Mfumo wa Kuufanya Udugu Uendelee kuwa Hai ...... 7
5. Mpango Mkakati Uliopendekezwa................. 9
6. Hitimisho na Mapendekezo ....10

Imetolewa na UEM .................11

# UTANGULIZI

Kongamano la tatu la kimataifa la Udugu la UEM lilifanyika mwezi Julai 2017 mjini Wuppertal, Ujerumani. Mada ya kongamano hilo ilikuwa, "Tangaza Habari Njema: Neema na Imani kwa njia ya Matendo." Wajumbe ishirini na nne kutoka Afrika, Asia na Ujerumani walijadiliana juu ya kazi za Udugu kwenye kongamano hilo. Kongamano lilijikita katika kutathmini utekelezaji wa tamko la Parapat na vipaombele vya Udugu kwa siku zijazo.

Kongamano la kwanza la kimataifa la Udugu lilifanyika mwaka 2007 mjini Dar es Salaam, Tanzania. Katika kongamano hilo, tathmini ya kazi au shughuli zote za Udugu kwa ujumla wake ilifanyika, huku msisitizo ukilenga theolojia na historia ya Udugu. Kongamano la pili la kimataifa la Udugu lilifanyika mjini Parapat, Indonesia mwaka 2012, mada ikiwa ni "Kuelekea katika Uimarishwaji wa Imani Yetu."

**NATAKA KUWASHIRIKISHA NINYI NYOTE FURAHA HIYO. HALI KADHALIKA NANYI MNAPASWA KUFURAHI NA MIMI NITAFURAHI PAMOJA NANYI.**

(WAFILIPI 2:17-18).

### Tathmini ya Tamko la Parapat

Tathmini ya tamko la Parapat juu ya Udugu ilirejewa na ilirekebishwa na kuwasilishwa na maofisa wa UEM na wajumbe kutoka mabara matatu yaani, Afrika, Asia na Ulaya (Ujerumani). Wakati makundi mengine ya Udugu yakiwa yamepiga hatua kubwa katika kutekeleza mpango mkakati wa mawasiliano, muundo wa Udugu, ushirikishwaji wa vijana na wanawake, mafunzo kupitia taasisi za ki-ekumene, miongozo ya Udugu, na miradi, bado kuna mambo mengi yaliyokusudiwa ambayo bado hayajatekelezwa. Utekelezaji wa tamko la Parapat unatakiwa uwe endelevu, mfano Udugu kati ya Asia na Afrika, udugu baina ya mabara matatu, kuajiri afisa mratibu wa mambo ya Udugu wa bara la Afrika n.k.


### Hatua za Kuzingatiwa katika Udugu

Baada ya kutathmini taarifa (tamko la) ya Parapat, na kuijadili na kupata mawazo mbali mbali juu ya taarifa ile, tukaona haja ya kuuongezea nguvu Udugu na kuufanya Udugu kuwa wenye furaha, ubunifu na ulio hai. Haya ni matokeo ya Kongamano la Kimataifa la Udugu. Kuanzia sura ya kwanza hadi sura ya nne zinazungumzia matokeo, mawazo mbali mbali, na motisha kutoka kwenye makundi manne ya washiriki wa kongamano toka mataifa mbali mbali. Sura ya tano na sura ya sita zinabeba mawazo mbali mbali kutoka kwenye makundi haya ya washiriki wa kongamano hili.


# 1. UDUGU WENYE FURAHA, UBUNIFU NA ULIO HAI UNAWEZEKANA! – "BWANA, UTUPE UJASIRI WA KUJENGA MADARAJA"

Pembetatu hii ya Udugu inatumika kama njia ya kuimarisha uhusiano kati ya makundi ya Udugu katika maeneo yao. Pembe tatu hii ya Udugu pia inaonyesha umuhimu au hitaji la uwiano kati ya muundo, hatua za utekelezaji(mchakato) na uaminifu. Kupitia mfano wa pembe tatu hii ya Udugu, kila kikundi cha Udugu kinapata nafasi ya kujitathmini.


Udugu ni uti wa mgongo wa UEM (rejea kwenye mwongozo juu ya Udugu: Kukua pamoja kama watu wa Mungu). Tumeungana pamoja na kuwa mwili mmoja katika Yesu Kristo kwa neema ya Mungu, kwa njia ya imani yetu na huduma yetu ulimwenguni. Ili tupate mafanikio kupitia Udugu, tunahitaji uwiano kati ya hatua za utekelezaji (mchakato), muundo na uaminifu. Kupitia uwiano wa jinsi hii, Udugu wetu utakuwa endelevu na utakuwa na uwezo wa kukabiliana na changamoto mbali mbali, mfano utofauti wa lugha na umbali uliopo kati yetu; uelewa tofauti tulionao juu ya misioni, utofauti wa mila na tamaduni zetu, utofauti wa historia zetu; utofauti juu ya matarajio tuliyonayo na utofauti wa kipato au kifedha n.k.



# 2. UPENDO KWA NJIA YA MATENDO







Tunakaribisha makundi ya Udugu kuutazama Udugu kwa ujumla au kwa ukamilifu wake. Mifumo yote mitano ya fahamu inapaswa itumike katika kuimarisha Udugu huu usio na ukomo tena Udugu wenye historia ya muda mrefu. Pia mifumo hiyo yote ya fahamu itumike katika kuanzisha mazungumzo mapya kwa lengo hilo hilo la kudumisha Udugu.

### Tumia Hisia (Moyoni)

Wadau wote wa Udugu wanatakiwa kuufurahia Udugu kutoka moyoni-mahusiano yaliyojaa upendo na furaha ndiyo msingi wa Udugu. Upendo ni msingi wa Udugu wowote. Upendo na uaminifu vikifanywa kuwa msingi wa Udugu, ndipo miongozo na makubaliano mengine yote vinafuatwa kwa urahisi.

### Tazama (Macho)

Miongozo na mikataba mbali mbali ya Udugu, ni mambo muhimu kwa Udugu. Hata hivyo wadau wote wa Udugu wanatakiwa kuzichukulia kanuni na miongozo si tu kama wajibu, bali pia kama fursa ya kuleta ubunifu katika masuala yote yanayohusu uimarishaji wa Udugu. Pia wadau wote wa Udugu wanatakiwa kuanza kuuona Udugu kwa mtazamo mpya wala si kuuona Udugu kama jambo la kihistoria tu au kama utamaduni tu, bali kama jambo endelevu na lenye kuleta msukumo kwa siku za usoni.

### Sikiliza (Sikio)

Wadau wote wa Udugu wanatakiwa kusikiliza mahitaji na uzoefu wa kundi au makundi ya Udugu wanayohusiana nayo. Hii ni pamoja na kuwa tayari kujifunza kutoka kwa wadugu hao, kisha watatakiwa kutafuta wataalam na washauri wa masuala husika kutoka miongoni mwa wadugu wanaohusiana nao.

### Kusema (Mdomo)

Wadau wote wa Udugu wamapaswa kuchagua na kujadiliana kwa pamoja mambo mbali mbali yenye maslahi kwa pande zote zinazohusika kwenye Udugu, mfano mambo yanayohusu maisha ya mijini, majanga, mambo yahusuyo familiya, mifumo ya elimu n.k

### Kunusa (Pua)

Wadau wa Udugu wanatakiwa kuwa na uelewa wa kutosha ili kufahamu mambo mbali mbali yahusuyo ufanisi wa shughuli mbali mbali za Udugu. Kila upande, yaani kila kundi la Udugu, linatakiwa kuwa na uelewa juu ya kundi wanalohusiana, hususani mahitaji, ndoto na maono ya kundi husika.

# 3. UMILIKI WA PAMOJA

Umiliki wa pamoja maana yake makundi husika ya Udugu yana mtazamo au maono ya pamoja na yanakubaliana kufanya kazi kwa pamoja ikiwa ni pamoja na kuchangia rasilimali zao katika kuyafikia maono. Ili kufikia lengo la umiliki wa pamoja wa Udugu, ni lazima kuwe na mabadiliko katika uwajibikaji. Mabadiliko hayo ni yale ya kutoka kwenye utegemezi kwenda kwenye kujitegemea ambako ni endelevu.

### Kuwa na Maono ya Pamoja

- Kuwa na maono ya pamoja kama makundi ya Udugu, ndiyo msingi wa udugu baina ya makundi husika.

- Makubaliano/mikataba/na kutimiza kwa vitendo ni mambo muhimu sana kwa Udugu.

- Kutafsiri neno "Udugu" katika mazingira na lugha ya kundi husika la Udugu, kunaongeza nguvu katika kuwa na maono ya pamoja juu ya Udugu, mfano "paralealeon" ni neno katika lugha ya Batak, lugha inayotumiwa na watu wa kaskazini ya Sumatra. Neno hili linamaanisha "urafiki wa moyoni." Lakini pia neno "Ubuntu" ni neno katika lugha za kibantu za Wazulu na Wakosa (Xhosa) katika bara la Afrika. Neno hili linamaanisha "Urafiki."

### Kuongeza Uelewa juu ya Udugu

- Waambie watu juu ya Udugu wenu. Mkutano au vikao vya Udugu viandae mhadhara utakaochangia katika kufanya habari mbali mbali zihusuzo Udugu ziwafikie watu kwa urahisi zaidi.

- Wadau wa Udugu wanatakiwa kuwa wawakilishi wa Udugu kwa washarika makanisani na kwenye matukio mbali mbali mfano sokoni, na kwenye skukuu mbali mbali za kanisa, n.k.

- Mahusiano ya umma ni muhimu na yanaweza kufanyika kupitia vyombo mbali mbali vya habari vya kijamii (tovuti, magazeti, vipeperushi, barua pepe na barua za kawaida)

### Miradi

- Lengo: kila kundi la Udugu litafaidika na miradi kwa namna moja au nyingine.

- Makundi ya Udugu yashirikishane kwa uwazi juu ya mahitaji ya makundi husika na kuhakikisha wanatafuta suluhisho la mahitaji hayo kwa pamoja.

- Tafadhali rejea kitabu cha UEM kinachotoa mwongozo juu ya miradi, "Upangaji wa Miradi ya Udugu" kisha tumia maelezo ya kitabu hiki katika kubuni na kupanga miradi, katika ufuatiliaji, na katika kutathmini miradi ya Udugu.

### Shirikisha Usharika Mzima

- Ibada za Udugu

  - Makundi mbali mbali ya Udugu yaandae kwa pamoja ibada maalum ya Udugu na kujumuisha mada mbali mbali zinazohusu Udugu ili zijadiliwe kwa pamoja. (Vifungu vya Biblia vinavyosisitiza umuhimu wa Udugu, sala, maombezi, nyimbo, sadaka kwaajili ya kuimarisha shughuli za Udugu vijumuishwe).

  - Kuwepo na kubadilishana kwa nyimbo zitakazoimbwa kwenye ibada hiyo maalum, au katika maonyesho ya uimbaji. Jumuisha washarika wote unapofanya harambee kwaajili ya kuchangia shughuli za maendeleo za Udugu.

### Ushirikishwaji wa Vijana katika shughuli za Udugu ili kuufanya Udugu kuwa endelevu


- Mahitaji ya vijana na jitihada zao vinatakiwa kuwa sehemu za mada za kujadiliwa kwenye mikutano ya Udugu. Vijana ni jamii ya watu wabunifu na watu muhimu katika kuleta mabadiliko katika jamii zetu. Vijana wengi hawaoni shida kuishi kwenye mazingira yenye watu wa tamaduni mbali mbali na kuwa kwenye udugu na watu hao. Mahusiano hayo yanabakia kuwa chachu ya mabadiliko. Kwahiyo lazima ubunifu utumike katika kuwavuta vijana ili waweze kuhusishwa na kushirikishwa katika shughuli mbali mbali za Udugu, mfano vijana wanaweza kupewa nafasi ya kutoa maoni yao juu ya Udugu wakiwa ndani ya kundi la Udugu, kwanjia ya kuanzisha makambi ya vijana na kwanjia ya nafasi mbali mbali za mafunzo yanayotolewa na taasisi mbali mbali za ki-ekumene. Udugu baina ya shule na shule utiliwe mkazo.

Mbali na hayo, makundi ya Udugu yatafanya mambo yafuatayo:

- Yatawafikia vijana kwenye madarasa yao ya kipaimara kwa kuwaalika wadau wa Udugu kufundisha juu ya Udugu kwenye madarasa hayo.

- Yatawafikia vijana kwenye madarasa yao ya shule za jumapili: Wadau wa Udugu pamoja na waalimu wa shule za jumapili, kwa pamoja watatakiwa kuandaa masomo ya shule za jumapili yanayogusa Udugu.

# 4. MFUMO WA KUUFANYA UDUGU UENDELEE KUWA HAI




Wanachama wote wa Udugu ni lazima wazingatie mzunguko au mfumo wa Udugu ili Udugu uwe wenye mafanikio, wenye furaha na wenye usawa. Hatua zifuatazo ni mahususi:

### Uchambuzi

- Sikiliza mahitaji ya kundi la Udugu unaloshirikiana nalo ili kuweza kufikia uelewa wa pamoja
- Zungumzeni kwa uwazi kabisa juu ya mahitaji mbali mbali yaliyopo na matarajio yenu
- Jadilianeni juu ya matarajio yenu.
- Zingatia uwepo wa uelewa tofauti juu ya Udugu, hivyo jadilianeni hadi mfikie uelewa wa pamoja juu ya maana halisi ya Udugu
- Tambua na uielewe kwa ukamilifu mada kamili ya kundi la Udugu unaloshirikiana nalo na mchango wa mada husika kwa kundi husika
- Zitambue changamoto za kundi la Udugu unaloshirikiana nalo, mfano utofauti wa lugha kama kikwazo kimojawapo, matatizo ya kifedha (ambalo ni tatizo pia kwa makanisa ya Ujerumani

### Panga Mkakati kwa Udugu wenu

- Unda malengo ya Udugu; malengo yaliyosheheni ubunifu lakini pia yaliyo rahisi na yasiyo na utata
- Shirikisha wadau mbali mbali ndani ya kundi lenu la Udugu, mfano vijana na ufanye kundi lenu la udugu kuwa lenye kuwavutia kwa kubuni shughuli mbali mbali zenyemvuto kwa vijana, mfano muziki, Sanaa na maigizo
- Udugu usibakie tu kwenye mazingira ya mikutano ya Udugu bali hata nje ya mikutano shughuli za Udugu ziendelee kutangazwa, ili na wengine waweze kujua na kushiriki
- Weka msisitizo katika ushirikiano wa ki-ekumene katika kujifunza juu ya mambo mbali mbali, maana sisi sote tu wakristo tunaokutana na changamoto za ulimwengu huu zinazofanana
- Shughuli mbali mbali zinazofanywa na makundi ya Udugu, zinatakiwa zitoe picha ya wajibu wa kanisa usio na mipaka
- Unda aina tofauti tofauti za ujumbe katika kutembeleana kupitia Udugu mfano viongozi wawakilishi wa Udugu, ujumbe kwa vijana, ujumbe kwaajili ya mashule.
- Udugu ni zaidi ya kutumiana taarifa (ripoti); Udugu unajumuisha mipango ya muda mrefu, mawasiliano ya kila wakati juu ya mambo mbali mbali, na uwajibikaji wa pamoja
- Uwe mfano mwema kwa jamii yako na kwa kundi lako la Udugu katika kufuata maadili ya kikristo

### Njia za Ziada Kuelekea kwenye Utekelezaji

- Pendekeza namna mpya ya kutekeleza mradi, mfano kundi moja na kundi jingine la Udugu iweni kundi la tatu shiriki katika ufadhili
- Undeni namna mpya ya Udugu, yenye ufanisi , mfano Udugu baina ya taasisi au baina ya makundi ya watumishi wa kada mbali mbali
- Kila jumapili na kwenye matukio mbali mbali, ombea makundi ya Udugu mnaohusiana nayo
- Fanya ziara zinazojumuisha watu wa tamaduni mbali mbali
- Imarisha Udugu baina ya Asia na Afrika
- Imarisha Udugu baina ya makundi mbali mbali kutoka kwenye mabara haya matatu, yaani Asia, Afrika na Ulaya (Ujerumani), huku pia ubunifu wa namna mbali mbali za udugu ukitiliwa mkazo

### Utekelezaji wa Mkakati na Njia za Ziada Kuelekea kwenye Utekelezaji

- Tekeleza mkakati na kwa uwazi kabisa uwashirikishe wadau wa Udugu unaoshirikiana nao juu ya changamoto unazokutana nazo
- Matatizo yakitokea wakati wa utekelezaji, lijulishe kundi la Udugu unaloshirikiana nalo tena kwa uwazi na kutafuta namna ya kutatua kwa pamoja
- Fuatilia na kutathmini mkakati wako na mbinu za ziada za utekelezaji. Uwe wazi kusema juu ya kusudio ulilonalo la ama kuufunga mradi au kuuongezea muda.



# 5. MPANGO MKAKATI ULIOPENDEKEZWA



**1.** UEM itasambaza matokeo au maazimio yaliyofikiwa na kongamano la kimataifa la Udugu la 2017 kwa makanisa yote wanachama wa UEM, kamati za Udugu na makundi yote ya Udugu

**2.** Makundi ya Udugu yatatengeneza mpango mkakati wa namna ya kuwasiliana hususani katika kupeana habari juu ya tathmini ya mahitaji ya makundi husika ya Udugu na rasilimali ambazo makundi haya husika yanazo

**3.** UEM, makanisa wanachama wa UEM, na makundi ya Udugu, yataandaa shughuli mbali mbali za Udugu wanazopenda kuzifanya lakini pia zinazozingatia maslahi ya wahusika, uwezo wa au taaluma ya wahusika, pamoja na usawa wa kijinsia n.k.

**4.** Makundi ya Udugu yatatakiwa kuwa wamiliki wa Udugu huku yakiendelea kuwahusisha washarika pamoja na watu wa dini mbali mbali pamoja na mashirika mbali mbali.

**5.** UEM itamwajiri mtu atakayeratibu shughuli zote zihusuzo Udugu kwa Bara la Afrika na atafanya kazi kwenye ofisi za UEM-Afrika pale Dar es Salaam

**6.** Makanisa na makundi ya Udugu yatawekeza kwenye shughuli mbali mbali za kujiingizia kipato ili kuweza kujitegemea.

**7.** Makanisa na makundi ya Udugu wataendeleza shughuli mbali mbali za Udugu kwa kuzingatia tamaduni za mahali husika.

**8.** UEM, makanisa wanachama wa UEM, na makundi ya Udugu, wote kwa pamoja wataongezea nguvu na msisitizo zaidi juu ya aina hii mpya ya Udugu (Udugu kati ya Asia na Africa, Udugu kati ya mabara matatu yaani Asia, Afrika na Ulaya-Ujerumani, Udugu unaojihusisha na mada au mkakati maalum na Udugu baina ya taasisi).



# 6. HITIMISHO NA MAPENDEKEZO

Sisi wajumbe wa kongamano la Udugu, tunatambua kwamba kazi ya Udugu inakabiliwa na changamoto mbali mbali katika nyakati hizi. Ili kuudumisha udugu na kujihusisha kikamilifu katika hili, tunawakaribisha wadau wote wa Udugu yaani UEM, Wanachama wote wa UEM, na makundi yote ya Udugu, kuyatumia maazimio yote yaliyofikiwa kwenye kongamano hili. Tunapenda kuhamasisha makundi yote ya Udugu yapokee maazimio haya na kuyajadili na kisha kuyatumia kama njia mpya ya kufanikisha Udugu pamoja na shughuli zote zinazofanywa kupitia Udugu.

### Wajumbe Kutoka Afrika

Rev. Eliki Bonanga – CDCC
Rev. Rose Marie Ibyishaka– EPR
Edna Kailembo – ELCT-KAD
Naomi Kisting – ELCRN
Polisi Kivava – CBCA
Rev. Dr Boniface Kombo – ELCT-ECD
Pierre Bruno Mbeumi – EEC
Leah Mongatane – ELCB

### Wajumbe Kutoka Asia

Rev. Herawaty Bangun – GBKP
K.K. Chan – CRC
Nathan Pahabol – GKI-TP
Manathaleo Quezon – UCCP
Rev. Merry Simarmata – HKBP
Arnest Sinaga – GPKB
Deborah Suparni – GKJTU
Rev. Fotani Ziliwu – BNKP

### Wajumbe Kutoka Ujerumani

Rev. Martin Ahlhaus – EKvW
Carolin Daubertshäuser – EKvW
Lisa-Marie Dummer – EKiR
Rev. Martje Mechels – EKiR
Rev. Christian Röhling – EKKW
Annette Salomo – EKvW
Rev. Matthias Ullrich – EKHN
Marion Unger – EKiR

### Wajumbe ambao ni Maafisa na Wafanyakazi wa UEM

Uli Baege
Gethsemane Bejaxhiu
Rev. Dr John Wesley Kabango
Rev. Jennie Keliat
Rev. Dr Muke Nagaju
Kristina Neubauer
Rev. Sonia Parera-Hummel
Elke Patalla
Rev. Petrus Sugito
Angelika Veddeler
David Wafo
Lena Wallraff

# IMETOLEWA NA UEM

**Imetolewa na UEM**

**Mchapishaji**
United Evangelical Mission (UEM)
Rudolfstrasse 137
42285 Wuppertal
Germany
✆ + 49 202 890 04 – 0
🖷 +49 202 890 04 -179
✉ info@vemission.org
www.vemission.org

**Mhariri**
Brunhild von Local

**Waandishi**
Wajumbe wote

**Maelezo**
Britta Kläffgen

**Mpangilio**
MediaCompany –
Agentur für Kommunikation GmbH

**Imechapishwa na**
Druckerei Hachenburg GmbH, Hachenburg

**Mzunguko**
300

**Uhariri**
Februari 2018

© United Evangelical Mission | Wuppertal, Februari 2018

DZI Spenden-Siegel
*Deutsches Zentralinstitut für soziale Fragen (DZI)*
***Zeichen für Vertrauen***

VEM